


HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

MKOA WA KILIMANJARO

Simu : 027-2758441
Fax : 027- 2756102



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

S. L.P. 27
HAI

Tarehe 01/09/2020

TANGAZO.

TANGAZO LA KUTAFUTA FUNDI KWA AJILI YA UKARABATI WA JENGO LA UTAWALA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai amepokea fedha kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Utawala lililopo Makao Makuu ya Wilaya.

Hivyo napenda kuwatangazia mafundi wote (local fundi) wenye uwezo wa kujenga/ au Kukarabati majengo ya serikali wajitokeze na kuomba kazi hii.

Mafundi wenye sifa na uzoefu wanatakiwa kuja kuchukua fomu maalumu(schedule of labour or dondoo shindani) katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kwa ajili ya kuzijaza bei za ukarabati wa jengo la Utawala lililopo Makao Makuu ya Halmashauri S.L.P.27 Hai.

Sifa za Mwombaji.

1. Awe ni raia wa Tanzania mwempe uelewa mzuri wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza
2. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
3. Awe na uelewa mzuri wa usalama na Afya awapo eneo la kazi.
4. Awe na timu ya kutosha ya mafundi mbalimbali kwa muda wote wa kazi mfano fundi mwashi, fundi bomba, fundi umeme, fundi carpenta nk.
5. Awe na uwezo wa kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa mradi /miradi na kumaliza kwa wakati.
6. Awe mwadilifu na mwaminifu.
7. Uwezo wa kusimamia mafundi wenzake na vibarua.
8. Mwenye zana zote muhimu za kazi (tools).


Uzoefu.

1. Uzoefu wa kuanzia miaka mitano na kuendelea katika kazi ya ujenzi.
2. Awe amefanya kazi yoyote ya ujenzi /ukarabati wa majengo ya serikali walau miradi mitatu na hati ya huduma (certificate of service) au mikataba ya miradi iliyotekelezwa ambayo inafikika kwa udhibitisho(ambatanisha udhibitisho).
3. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri mchoro/michoro ya majengo kwa lugha ya kiufundi.

Maombi yote yawekwe katika bahasha iliyofungwa vizuri na kuandikwa anuani ifuatayo., Mkurugenzi Mtendaji ,Halmashauri (W) Hai.S.L.P 27 Hai.

Mwisho wa kupokea maombi haya ni saa nane mchana (8.00) siku ya Ijumaa ya tarehe **04/09/2020** sehemu ya kuwasilisha maombi hayo ni ofisi ya Manunuzi na Ugavi S.L.P 27 Hai. Ufunguzi wa maombi hayo utafanyika tarehe **04/09/2020** katika ukumbi wa Halmashauri mbele ya waombaji watakaopenda kuhudhuria ufunguzi huo.

Tangazo limetolewa na



Elia Machange.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
HALMASHAURI YA WILAYA-HAI.

Kny. MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HAI